*Wekeza na jenga maisha na SACCOS*

# LESA SACCOS LTD

## REG. No DSR 1299

# SERA YA MIKOPO

WEKA AKIBA MARA KWA MARA, KOPA KWA BUSARA LIPA KWA WAKATI, WEKEZA KWA MAENDELEO YAKO.

TOLEO LA III 2020

## UIDHINISHAJI WA SERA YA MIKOPO

| **Tarehe ya Kupitishwa na Kikao Cha Bodi** | | | | **Kikao Cha Bodi**<br>**Tarehe 17 Julai 2020** |
|---|---|---|---|---|
| **Mpya**<br><br>**Imehuishwa** | | | ☐<br><br>☐ | **Toleo la; I**<br>**Mwaka 2020** |
| **Imetiwa Saini kwa Niaba ya Wanachama na;** | | | | |
| **S/N** | **Jina** | **Wadhifa** | **Tarehe** | **Sahihi** |
| 1 | EVA. J. BOSCO | Mwenyekiti wa Bodi | 23/11/2020 | |
| 2 | GWAMAKA JAPHARI | Mjumbe wa Bodi | 23/11/2020 | |
| 3 | SEMALY KISAMO | Mjumbe wa Bodi | 23/11/2020 | |
| 4 | SHAFII MMILE | Mjumbe wa Bodi | 23/11/2020 | |
| 5 | NAOMI SERBANTEZ | Mjumbe wa Bodi | | |

| **Imetiwa Saini kwa Niaba ya Watendaji na:** | | | |
|---|---|---|---|
| **Jina** | **Wadhifa** | **Tarehe** | **Sahihi** |
| DEONATUS KIHEKA | Meneja | | |
| **Kwa Matumizi ya Mrajis:** | | | |
| Maoni ya Mrajis: | | | |
| | | | |
| **Jina** | **Wadhifa** | **Tarehe** | **Sahihi** |
| | | | |
| *Muhuri* | | | |

## YALIYOMO

1.1 UTANGULIZI ..... 3
1.2 MADHUMUNI YA SERA YA MIKOPO ..... 4
1.3 WALENGWA WA SERA YA MIKOPO ..... 4
1.4 WADAU WA NDANI ..... 5
1.5 WADAU WA NJE ..... 5
1.6 MISINGI YA SERA ..... 5
1.7 UPEMBUZI WA MIKOPO YA LESA SACCOS LTD ..... 6
1.8 SIFA ZA JUMLA MWANACHAMA KUPATA MKOPO ..... 7
1.9 TARATIBU MAHSUSI ZA UTOAJI MIKOPO ..... 13
**1.10 USALAMA WA MIKOPO** ..... 16
1.11 DHAMANA NA UDHAMINI ..... 16
**1.12 ENEO DHAMANA ILIPO** ..... 17
1.13 UKOMO WA DHAMANA ..... 17
1.14 KUJITOA UANACHAMA NA MAEJESHO YA MKOPO ..... 18
1.15 UFUATILIAJI WA MWENENDO WA MIKOPO ..... 18
1.16 MAOMBI YA MKOPO ..... 18
1.17 KUIDHINISHA NA KUKUBALIWA KWA MAOMBI YA MKOPO ..... 19
1.18 MAMLAKA YA KUIDHINISHA MIKOPO ..... 20
1.19 MIKOPO KWA VIONGOZI NA WATENDAJI ..... 21
1.20 KUREJESHA MIKOPO ..... 22
1.21 MUDA NA UTARATIBU WA MAREJESHO ..... 22
1.22 MENEJIMENTI YA MAJANGA YA MIKOPO ..... 22
1.23 NJIA YA KUKOKOTOA RIBA ..... 23
1.24 UFUATILIAJI WA MAREJESHO YA MKOPO ..... 23
1.25 MAREJESHO YA MIKOPO ILIYOCHELEWA ..... 24
1.26 UMRI WA MIKOPO ..... 24
1.27 MATENGO YA MADENI MABAYA ..... 25
1.28 TAARIFA ZA MIKOPO ..... 26
1.29 TARATIBU ZA KUFUATILIA MIKOPO ILIYOCHELEWA ..... 26
1.30 MATUMIZI YA DALALI ..... 27
1.31 HAKI JUU YA DHAMANA ..... 29
1.32 UFUTAJI MIKOPO ..... 29
1.33 UFUATILIAJI MKOPO BAADA YA KUFUTWA VITABUNI ..... 31
1.34 NAFASI YA MAHAKAMA KUPITIA TARATIBU ZA TUME ..... 31
1.35 MAREKEBISHO YA MKOPO ..... 31
1.36 UHUISHAJI WA SERA ..... 32

## 1.1 UTANGULIZI

LESA SACCOS LTD ilianzishwa kwa kuzingatia Sheria ya Vyama Vya ushirika Na.20 ya mwaka 2003.Kwa malengo ya kupokea akiba na kutoa Mikopo yenye masharti nafuu kwa wamanachama wake. Mkutano mkuu wa wanachama ndicho chombo cha juu chenye mamlaka katika shughuli zote za chama na kwa kuzingatia Sheria ya Vyama Vya ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 kinatambua kuwa bodi ya chama ndio chombo pekee cha kuongoza chama kwa kuzingatia ukasimishwaji wa madaraka hayo kupitia mkutano mkuu wa wanachama.
Kifungu Na.52 cha Sheria ya Vyama Vya Ushirika kinaenda mbali zaidi na kutoa nafasi kwa bodi kuandaa miongozo mbalimbali ya kusimamia chama na miongoni mwa miongozo iliyotajwa ni pamoja na sera ya mikopo.

Sera ya Utoaji, ukusanyaji na ufutaji wa mikopo ya LESA SACCOS LTD ni mwongozo uliowekwa na chama kwa ajili ya kusimamia namna ya utoaji wa mikopo ndani ya chama na ni ramani ya chama inayoonesha namna ya kutoa mikopo kwa wanachama wake. Taratibu hizi za mikopo zimetungwa kwa kuzingatia misingi ya kanuni za utendaji bora wa chama na lazima zifuatwe na zitumike katika shughuli zote za utoaji mikopo kwa wanachama.

Sera hii itazingatia matakwa ya Sheria ya Sheria ya vyama vya ushirika Na.6 ya mwaka 2013, Kanuni za vyama vya ushirika za mwaka 2015 pamoja na Sheria ya Huduma ndogo za fedha Na.10 ya mwaka 2018 na Kanuni za Huduma ndogo za fedha za mwaka 2019. Sera hii imejumuisha Maeneo yote muhimu yanayopaswa kuzingatiwa katika usimamizi wa mikopo ikiwa ni pmoja na utoaji wa mikopo, Ukusanyaji wa Mikop, Ufutaji wa Mikopo, Dhamana za mkopo, taratibu za kuuza dhamana, bima ya mikopo, kama zinavyoelekezwa katika Kanuni ya 28-43 ya Kanuni ya huduma ndogo za fedha za mwaka 2019.

Sera hii imejumuisha Sehemu kumi na tatu. Sehemu ya kwanza ni utangulizi, sehemu ya pili ni utoaji wa mikopo na taarifa ya kukataliwa kupewa mkopo, sehemu ya tatu ni gharama za mkopo, sehemu ya nne ni bima ya mkopo, sehemu ya tano ni muda kikomo wa marejesho ya mkopo, sehemu ya sita ni vyanzo vya kukopesha na ukomo wa ukopeshaji, sehemu ya saba ni uidhinishaji wa maombi ya mkopo na

urejeshaji wa mkopo, sehemu ya nane ni ukokotoaji na uainishaji wa mikopo iliyocheleweshwa, sehemu ya tisa usitishaji wa mapato tarajiwa wa marekebisho ya mkopo, sehemu ya kumi ni madeni, matengo na usimamishaji wa mikopo kwa muda, sehemu ya kumi na moja ni ukusanyaji wa madeni, sehemu ya kumi na mbili ni ufutaji wa mkopo na uazaji wa dhamana na sehemu ya kumi na tatu ni muda wa rehema katika kulipa mkopo.

Sera hii imeandaliwa kwa kuzingatia sharti Na. la masharti ya chama, pamoja na mambo mengine sera hii itapitiwa mara kwa mara ili kuona kama kunahitaji la kufanya maboresho na bodi itakuwa na jukumu la kuwasilisha maoni na mapendekezo katika maeneo watakayoona yanafaa kwa lengo kuridhiwa na mkutano mkuu kabla ya kufanya maboresho.

## 1.2 MADHUMUNI YA SERA YA MIKOPO

(a) Kuweka misingi na kanuni bora za utoaji mikopo.
(b) Kuepusha migongano isiyo ya lazima katika kutoa mikopo.
(c) Kupunguza hatari ya mikopo mibaya.
(d) Kujenga imani kwa taasisi za ndani na nje, wanachama na wananchi kwa ujumla.
(e) Kuiwezesha Bodi katika usimamizi wa mikopo.
(f) Kutekeleza kwa vitendo Sheria ya Huduma ndogo za fedha Na.10 ya mwaka 2018 na Kanuni za Huduma ndogo za fedha za mwaka 2019.

## 1.3 WALENGWA WA SERA YA MIKOPO

Walengwa wa sera hii ni wanachama wale wote watakaokuwa wakihusika na mikopo kwa namna moja ama nyingine ikiwa ni pamoja na waombaji, wapitiaji, waidhinishaji, na wasimamiaji wa mikopo ya LESA SACCOS LTD. Pamoja na wengine watakaohusika na sera hii kwa namna moja ama nyingine, sera itawahusu moja kwa moja wafuatao: -

(1) Wanachama, viongozi wa Bodi na Kamati ya Usimamizi.
(2) Watendaji.

(3) Wasimamizi wa Sheria za Ushirika (wakati wote huhakiki uhalisia wa utoaji huduma za mikopo kama unaendana na taratibu zilizokubaliwa ndani ya Sera hii).

## 1.4 WADAU WA NDANI

(i) Wanachama ndio walengwa wakuu wa Sera hii kwa kuwa ndio wakopaji
(ii) Watendaji – Hawa ni wataalamu wa kuchanganua na kutathmini mikopo inayoombwa na inayotolewa.
(iii) Wajumbe wa bodi, Kamati ya usimamizi – watahusika katika kusimamia na kuhakikisha kuwa taratibu zote za Sera zinafuatwa.

## 1.5 WADAU WA NJE

i) Wakaguzi wa nje – Watatumia Sera hii wakati wa ukaguzi.
ii) Maafisa ushirika – Ni washauri katika utekelezaji wa sera hii kama wawakilishi wa Serikali.
iii) Taasisi za Kifedha na wakopeshaji wengine – Watatumia sera hii wakati wa kutoa huduma ya mikopo chamani.
iv) Mrajis wa Vyama vya Ushirika – anahusika na kuidhinisha sera hii na kusimamia utekelezaji wake.
v) Makampuni ya kuchakata taarifa za wakopaji
vi) Waajiri
vii) Benki kuu ya Tanzania
viii) Wadau wengine

## 1.6 MISINGI YA SERA

Katika kuandaa sera hii, mambo yafuatayo yatazingatiwa, pamoja na hali halisi ya mfumo wa uchumi: -
(a) Sheria ya vyama vya Ushirika ya mwaka 2013, na kanuni zake za mwaka 2015, Sheria ya huduma ndogo za fedha na kanuni zake.
(b) Masharti ya Chama;
(c) Sheria za kazi;
(d) Sheria ya ardhi na makazi;

(e) Sheria, taratibu na kanuni za utumishi

## 1.7 UPEMBUZI WA MIKOPO YA LESA SACCOS LTD

Katika taratibu za ukopeshaji wa Mikopo ya LESA SACCOS Ltd, Misingi ifuatayo itazingatiwa.

### 1.7.1 TABIA YA MKOPAJI

Tabia ya mkopaji lazima itathiminiwe kulingana na ubora wake binafsi na kumbukumbu zake za mikopo. Wanachama, Kamati ya Usimamizi, Kamati ya mikopo au kiongozi yeyote wa chama anayemfahamu mkopaji anaweza kufanya tathimini ya tabia yake katika kurejesha mikopo. Dhamana kubwa iliyopita kiwango cha mkopo isiwe kigezo cha kumpa mkopo mwanachama aliye na tabia mbaya. Wakopaji wapya watatathiminiwa kwa kuzingatia uwezo wao wa marejesho na tabia katika jamii na mahusiano kazini.

### 1.7.2 HALI

Hali itazingatia mambo ya nje yanayoathiri mkopo wa mwombaji;-

(i) Hali ya uchumi wa nchi.

(ii) Thamani ya pesa.

(iii) Sheria za nchi.

(iv) Hali ya soko la biashara inayoombewa mkopo.

(v) Hali ya soko la ajira.

(vi) Upatikanaji wa fedha.

### 1.7.3 UWEZO NA MTIRIRIKO WA FEDHA

Uwezo wa kurejesha ndio kitu cha kwanza cha kuangalia katika kutathimini mkopo. Hii ni kanuni muhimu sana katika kuchanganua mkopo.

### 1.7.4 DHAMANA

Kwa mujibu wa Kanuni ya 33(1) ya huduma ndogo za fecha, sharti kila mkopo uwe umedhaminiwa kikamilifu. Hivyo kutawekwa mfumo wa dhamana ambayo Mwanachama lazima aweke ili kutimiza vigezo vya kupatiwa mkopo. Thamani ya dhamana lazima iwe zaidi ya 100% ya thamani ya mkopo anaoombwa.

### 1.7.5 KINGA DHIDI YA MAJANGA

Mikopo inasongwa na majanga mbalimbali ikiwemo kifo, ulemavu wa kudumu, kufukuzwa ama kupunguza kazini, kufa kwa biashara kutokana na sababu mbalimbai n.k. Hivyo, ili Chama kijihakikishie kiko salama lazima kuwe na kinga thabiti dhidi ya majanga yoyote yatokanayo na mkopo. Kinga hiyo kwa kiwango kikubwa itakuwa katika mfumo wa Bima ya Mikopo na dhamana zake rejea será ya majanga.

## 1.8 SIFA ZA JUMLA MWANACHAMA KUPATA MKOPO

Ili kuweka mazingira mazuri ya kuhakikisha mikopo inatolewa baadhi ya mambo yafuatayo yatazingatiwa kabla mwanachama hajapatiwa mkopo ambapo mwanachama ni lazima awe na sifa zifuatazo;

(a) Awe mwanachama hai wa LESA SACCOS LTD anayechangia Akiba yake isiyopungua Tsh.60,000 kila baada ya wiki mbili, Mwenye Hisa angalau 100 zenye thamani ya Tshs.1,000,000 na zinazobaki atazikamilisha ndani ya kipindi cha miezi ishirini nan ne (24) kama inavyoelekezwa na sera ya uhamaishaji uwekaji akiba amana na hisa.

(b) Awe ametimiza miezi mitatu chamani tangu kujiunga kabla ya kuomba huduma ya mkopo chamani.

(c) Asiwe na mkopo alioshindwa kulipa wakati wa kuomba mkopo mwingine.

(d) Asiwe na mkopo alioshindwa kulipa kutoka taasisi nyingine.

(e) Awe na historia nzuri chamani katika urejeshaji wa mikopo yake.

(f) Awe mshiriki mzuri kwenye shughuli za chama.

(g) Awe na dhamana toshelevu, mdhamini na wadhamini ikiwa akiba zake, hisa za hiyari na amana hazijitoshelezi kudhamini mkopo anaomba.

**Pamoja na sifa zilizoainishwa katika sehemu hii pia mambo yafuatayo yatazingatiwa kama sifa ya mwanchama kuweza kupatiwa mkopo**

## AKIBA NA HISA

Akiba na hisa za mwanachama zilizowekwa chamani zitazingatiwa na kuwa kigezo muhimu cha kutoa mkopo kwa mwanachama na ikiwa mwanchama hajatimiza sharti la kuwa na hisa na kuweka akiba kama taratibu zinavyoelekeza katika sera ya uhamasihaji wa uwekaji akiba na hisa anaweza kukosa sifa ya kupata mkopo.

## TABIA (CHARACTER)

Tabia ya mkopaji itathiminiwa kikamilifu kulingana na kumbukumbu zake za ukopaji na urejeshaji wa mikopo yake. Wanachama, Kamati ya Usimamizi, Kamati ya mikopo au kiongozi yeyote wa chama anayeweza kuwa sehemu ya kujua tabia ya mkopaji na anaweza kutoa maoni juu ya mkopaji husika.

Dhamana kubwa iliyopita kiwango cha mkopo haitakuwa kigezo cha kumpa mkopo mwanachama aliye na tabia au historia mbaya katika ukopaji na urejeshaji wa mikopo.

Wakopaji wapya watatathiminiwa kwa kuzingatia uwezo wao wa kufanya marejesho.

## HALI (CONDITION)

Hali ya utoaji wa mkopo kwa mwanachama itazingatia mambo ya nje yanayoathiri mkopo wa mwombaji ikiwa ni pamoja na

i. Hali ya uchumi wa nchi
ii. Thamani ya pesa
iii. Hali ya soko la biashara inayoombewa mkopo
iv. Hali ya soko la kazi/ajira
v. Mambo mengine yanayoathiri hali ya urejeshaji mkopo.

## UWEZO WA MTIRIRIKO WA KIFEDHA

Uwezo wa kurejesha mkopo ndio kitu cha kwanza na cha msingi cha kuangalia katika kutathimini uwezo wa mwanachama kurejesha mkopo anaoomba kwa kutegemea shughuli za kiuchumi

## DHAMANA YA MKOPO (COLLATERAL)

Dhamana itakayowekwa/zitakazowekwa na mwanachama wakati wa kuomba mkopo zitatakiwa kuwa na thamani zaidi ya kiwango cha mkopo utakaoombwa. Aidha, tathmini halisi ya thamani ya dhamana itakayowekwa na wanachama itatakiwa kutathiminiwa vizuri kabla ya kuwekwa kwenye dhamana ya mkopo kwa gharama ya mkopaji. *(Mthaminishaji anayetambuliwa na serikali).*

### 1.8.1 AINA YA MIKOPO INAYOTOLEWA NA CHAMA

LESA SACCOS LTD ina aina NNE (4) za Mikopo yenye malengo mbalimbali kama ifuatavyo:

### 1.8.2Mkopo wa chap chap (Express Loan)

(a) Kiwango cha chini ni Shilingi 50,000/= (Elfu Hamsini) na kiwango cha juu ni Shilingi 2,000,000/=(Millioni mbili tu).

(b) Hutolewa kipindi chochote ili mradi pawepo na fedha katika chama. Si lazima zisubiri kikao cha kamati ya mikopo bali inaweza kuidhinishwa na Afisa Mikopo na Meneja na kutoa taarifa kwenye kikao cha Kamati ya Mikopo na Bodi kinachofuata.

(c)Mwanachama anaweza kukopa mkopo wa chap chap hata kama ana mikopo mingine ya aina nyingine ili mradi tu awe na uwezo wa kulipa.

(d) Mkopo huu unatolewa ndani ya siku moja.

(e) Marejesho ya mkopo huu yatafayika ndani ya miezi mitatu (mwezi wa tatu baada ya kupokea mkopo) na yatafanyika kwa kuweka fedha benki kwenye akaunti ya chama na kisha kuwasilisha *slip* ya muamala huo kwa meneja.

(f) Marejesho yataambatana na riba ya asilimia kumi (10%).

(g) Mwanachama ambaye hatarejesha mkopo huu wakati uliopangwa na chama hatatakiwa kupewa mkopo mwingine

wowote mpaka atakapokamilisha marejesho ya awali. Hii pia itaathiri maombi yoyote ya mikopo kutoka kwa mwanachama husika.

### 1.8.3 Mkopo wa dharula (Emergency Loan)

(a) Kiwango cha chini cha kukopa ni shs. 500,001/= (laki tano na moja) na kiwango cha juu ni Shs. 10,000,000/= (Milioni kumi)

(b) Mkopo huu utategemea uwezo wa mwanachama kimshahara kurejesha.

(c) Hutolewa kipindi chochote ili mradi pawepo na fedha katika chama si lazima usubiri kikao cha kamati ya mikopo bali inaweza kuidhinishwa na Afisa Mikopo na Meneja na kutoa taarifa kwenye kikao cha Kamati ya Mikopo na Bodi kinachofuata.

(d) Mwanachama anaweza kukopa mkopo wa dharura hata kama ana mkopo mwingine wa aina nyingine ili mradi tu salio la mshahara wake linaruhusu kukatwa ndani ya miezi miezi kumi na mbili (12).

(e) Mkopo huu hautatolewa kwa mwanachama ambaye atakuwa hajarejesha mkopo wake wa awali (mkopo wa dharula) wote kikamilifu.

(f) Makato ya mkopo wa dharura yatafanyika ndani ya kipindi cha miezi kumi na mbili. Si ruhusa kuongeza muda wa marejesho ya mkopo wa dharura ili kutoa nafasi kwa wakopaji wengine.

(g) Riba ya mkopo wa dharula ni asilimia 14% kwa mwaka kwa baki ya mkopo (reducing balance method) au kama itakavyokuwa inarekebishwa mara kwa mara kufuatana na hali ya uchumi.

(h) Mwanachama ambaye hatarejesha mkopo huu kwa wakati uliopangwa na chama, hatatakiwa kupewa mkopo mwingine wowote mpaka atakapokamilisha marejesho ya awali. Hii pia itaathiri maombi yoyote ya mkopo kutoka kwa mwanachama husika.

## 1.8.4 Mkopo wa maendeleo (Development Loan)

(a) Mkopo huu utatokana na akiba za wanachama. Mkopo huu utakopeshwa kwa madhumuni ya ujenzi, ufugaji, upanuzi wa mashamba, viwanda vidogo, ununuzi wa nyumba na vyombo vya usafiri na maendeleo mengine.

(b) Mwanachama anaweza kukopa kiwango ambacho hakitazidi mara tatu (3) ya akiba zake katika chama.

(c) Kiwango cha juu kabisa cha kukopa ni Sh. 60,000,000/= (Milioni Sitini kamili tu) pia itategemea akiba na hisa za mwombaji zilizopo katika chama na uwezo wa mkopaji (mshahara wa mwanachama husika, madeni katika mabenki na taasisi binafsi alizokopa).

(d) Muda wa kurejesha mkopo huu ni ndani ya miezi sitini (miaka nitano) kulingana na matakwa ya mwanachama husika.

(e) Mwanachama anaweza kukopa tena iwapo atakuwa amekwishalipa theluthi mbili (2/3) ya mkopo wa awali au awe amemaliza kabisa deni.

(f) Ni ruhusa kwa mwanachama kutunisha akiba na hisa zake katika chama kwa kuingiza fedha taslim katika chama kupitia benki kwenye akaunti ya chama. Mwanachama atatakiwa kupeleka karatasi ya benki iliyotumika kuwekea fedha kwenye akauti ya chama (bank depost slip) kwa mhasibu wa chama au mtunza fedha wa chama, naye kubakiwa na nakala yake. Mhasibu atazirekodi akiba mpya za mwanachama pale atakapothibitisha kwamba pesa imeingia katika akaunti ya chama na kumwandikia stakabadhi (Receipt) ya kupokea fedha hizo. Ni vizuri wanachama wakaelewa

tofauti ya kutunisha akiba na ***dumping*** ya fedha kwenye account ya SACCOS kwa madhumuni ya kukopa. Kamati ya mikopo itapitia maombi yote na kufanya upembuzi yakinifu kujua endapo ***deposit*** hiyo ni **dumping** au ni kwa nia ya kutunisha akiba. ***Dumping*** haikubaliki kwa kuwa inavuruga mtiririko wa fedha kwa chama hasa pale wanaofanya dumping wanapokopa.

(g) Baada ya kutunisha akiba, mwanachama atalazimika kukaa miezi miwili kwanza kabla ya kukopa. Hii itatoa nafasi kwa kamati ya mikopo, usimamizi na bodi ya chama kuthibitisha akiba mpya ya mwanachama.

(h) Riba ya mkopo wa maendeleo ni asilimia 14% kwa mwaka kwa baki ya mkopo (reducing balance method) au kama itakavyokuwa inarekebishwa mara kwa mara kufuatana na hali ya uchumi.

### 1.8.5 Mkopo Mkubwa (Super Loan)

(a) Mkopo huu utatokana na akiba ya mwanachama. Mkopo huu utakopeshwa kwa madhumuni ya ujenzi ufugaji, upanuzi wa mashamba, viwanda vidogo, ununuzi wa nyumba na vyombo vya usafiri na maendeleo mengine.

(b) Huu ni mkopo wa kiwango cha kuanzia Shilingi 61,000,000/= (Milioni sitini na moja) hadi shilingi 100,000,000/= (Milioni Mia Moja) kiwango cha juu.

(c) Mkopo huu pia utatolewa kwa kuzingatia akiba za mwanachama, DCF na uwezo wa mwanachama kurejesha kupitia mshahara wake.

(d) Mkopo utarejeshwa ndani ya miezi 60 (miaka mitano), kulingana na matakwa ya mwanachama.

(e) Mwanachama anaweza kukopa tena iwapo atakuwa amekwishalipa theluthi mbili (2/3) ya mkopo wa awali au awe amemaliza kabisa deni.

(f) Ni ruhusa kwa mwanachama kutunisha akiba zake katika chama kwa kuingiza fedha taslimu katika chama kupitia akaunti yake ya mshahara au kwa kuweka fedha benki kwenye akaunti ya chama. Mwanachama atatakiwa kupeleka karatasi ya benki iliyotumika kuwekea fedha kwenye akaunti ya chama (bank deposit slip) kwa mhasibu wa chama au mtunza fedha wa chama, na yeye kubakiwa na nakala yake. Mhasibu atazirekodi akiba mpya za mwanachama pale watakapothibitisha kwamba pesa imeingia katika akaunti ya chama na kumwandikia stakabadh (Receipt) ya kupokea fedha hizo.

(g) Baada ya kutunisha akiba, mwanachama atalazimika kukaa miezi miwili kwanza kabla ya kukopa. Hii itatoa nafasi kwa kamati ya mikopo, usimamizi, na bodi ya chama kuthibitisha akiba mpya ya mwanachama.

(h) Riba ya super loan ni asilimia 14% kwa mwaka kwa baki ya mkopo (reducing balance method) au kadri itakavyokuwa inarekebishwa mara kwa mara kufuatana na hali ya uchumi.

## 1.9 TARATIBU MAHSUSI ZA UTOAJI MIKOPO

a. Mikopo itatolewa kwa wanachama hai tu ambao wanatambulika kisheria na kwa kulingana na masharti ya LESA SACCOS LTD na kwamba kila mwanachama atakuwa

na haki ya kupata mkopo kulingana na sheria, kanuni na sera bila kujali cheo chake.

b. Mwanachama mpya ataruhusiwa kupata mkopo baada ya kulipa kiingilio, hisa na kuweka akiba walau kwa kipindi kisichopungua miezi mitatu (3).
c. Maombi yote ya mikopo lazima yawe katika maandishi. (Mwombaji lazima ajaze fomu ya mkopo). Fomu ieleze wazi malengo ya mkopo, kiasi kinachoombwa, na muda wa marejesho.
d. Mwombaji wa mkopo na wadhamini wasiopungua wawili watasaini barua/makubaliano maalumu (*Commitment letters*) zitakazosainiwa na ofisi ya Mwajiri wa mkopaji.
e. Maombi yote ya mikopo yataidhinishwa na kamati ya mikopo katika kikao cha pamoja kitakachokuwa kinafanyika mara kwa mara kulingana na mahitaji ya wanachama. Afisa mikopo atakuwa katibu wa kamati hiyo naye pamoja na meneja wataidhinisha mikopo ya dharura.
f. Maombi ya mikopo ya wajumbe wa Bodi yatafikiriwa na kikao cha pamoja cha wajumbe wa Bodi ila mwombaji hatashiriki katika kikao kitakachojadili maombi yake.
g. Riba ya mkopo itakokotolewa kwa njia ya baki ya mkopo (reducing balance method) au kadri itakavyokuwa inarekebishwa mara kwa mara kwa kiwango chote cha mkopo.
h. Mikopo ya maendeleo lazima ikatiwe bima isipokuwa mikopo ya dharula na chap chap.
i. Kamati ya mikopo itatakiwa kuhakikisha kuwa katika hali ya kawaida jumla ya makato kwa ajili ya marejesho ya mkopo wa mwanachama hayatazidi asilimia sitini (60%) ya mshahara wake.
j. Mwanachama atawajibika kulipia Hisa angalau 100 zenye thamani ya Tshs.1,000,000 na zinazobaki atazikamika kulipia ndani ya kipindi cha miezi ishirini na nne (24) kama inavyoelekezwa na sera ya uhamaishaji uwekaji akiba amana na hisa. Aidha mwanachama atatakiwa awe ameweka akiba inayomwezesha kukopa hadi mara tatu (3) kiwango cha juu cha akiba zake.

k. Mwanachama ambaye ana historia mbaya ya kurejesha mkopo, hawezi kupewa mkopo mpaka itakapothibitishwa na bodi kuwa sababu zilizomfanya ashindwe/acheleweshe mkopo wa nyuma hazipo tena.
l. Endapo akiba, hisa na mali zilizokamatwa haziwezi kufuta deni lote, kiasi kilichosalia kitalipwa na wadhamini wa mkopaji.
m. Kwa mikopo yote, mwanachama mmoja hataruhusiwa kukopa kiasi kinachozidi 10% ya jumla ya hisa za hiari na akiba zote za wanachama kwa wakati mmoja.
n. Mwanachama mmoja haruhusiwi kudhamini zaidi ya **wakopaji wawili** na dhamana moja hairuhusiwa kutumika zaidi ya mkopo mmoja. Kamati ya mikopo inatakiwa kuthibitisha hili.
o. Kamati ya mikopo ina jukumu la kutathimini maombi mbalimbali ya mikopo kwa wanachama na kuhakikisha kwamba mikopo inayotolewa haikiuki masharti ya chama na sera ya mikopo ya chama. Kamati ya usimamizi utashauriana na bodi ili kuhakikisha kwamba mikopo yote inarudishwa kwa wakati uliopangwa kwenye mkataba.
p. Ili kuhakikisha kuwa sera ina tija, Bodi itashauriana na Kamati ya Mikopo na Kamati ya mikopo kila wakati kuhakikisha kwamba, wakati wote sera ndiyo inayoongoza utoaji wa mikopo na suala la utashi binafsi katika suala la mikopo halipewi nafasi na linadhibitiwa.
q. Mikopo ya chap chap na dharura itaidhinishwa na meneja na kisha kupelekwa kwa mwenyekiti au makamu na mikopo hii itatolewa kwa waombaji waliotangulia kwanza (First In, First Served). Hii ina maana kwamba maombi yaliyotangulia ndiyo yatakayoshughulikiwa kwanza. Hivyo, maombi yote yanayopokelewa yatawakewa namba na tarehe ya kupokelewa, na kufailiwa kwa mtindo wa yaliyoingia kwanza kuwa juu.

## 1.10 USALAMA WA MIKOPO

Kwa mwanachama atakayeshindwa, atakayekataa au atakayechelewesha marejesho kiasi cha kutaka kuathiri usalama wa mikopo, chama kinaweka kinga kama ifuatavyo: -

i. Mkopo utatolewa kulingana na uwezo wa kulipa wa mkopaji na kila mkopo lazima udhaminiwe kikamilifu na dhamana.
ii. Uwezo wa wadhamini wa kulipa deni lote au upungufu wa fedha inayodaiwa na chama kutoka kwa mkopaji.
iii. Tengo la kinga ya madeni mabaya katika bajeti ya chama ya kila mwaka.
iv. Chama kukata bima ya kinga ya mikopo yote itakayokuwa mikononi mwa wanachama dhidi ya janga.

## 1.11 DHAMANA NA UDHAMINI

**Dhamana ya mkopo:**

Mikopo yote itatolewa baada ya Kamati ya mikopo kutathimini na kujiridhisha uwepo, uhalali, umiliki na thamani halisi ya dhamana iliyowekwa. Ufuatayo ni utaratibu na aina za dhamana; -

(i) Dhamana juu ya mikopo inaweza kuwa ni akiba na hisa za hiari za mkopaji, na mali isiyohamishika au dhamana nyinginezo kama zitakavyoombwa na Kamati ya Mikopo kutokana na upembuzi wa mkopo husika.
(ii) Kama mwanachama ameweka dhamana ya mali isiyohamishika, kabla ya mkopo kutolewa lazima dhamana husika ifanyiwe "search" kuona kama ni halali, haina madeni na haijawekwa dhamana kwenye taasisi nyingine za fedha, baada ya kujiridhisha sharti dhamana isajiriwe ili Chama kiwe na sehemu ya umiliki ama kuwa na mamlaka juu ya dhamana hiyo.
(iii) Mali za mkopaji.
(iv) Akiba na hisa za hiari za wadhamini.
(v) DCF ya mkopaji.

**Wadhamini:**

(i) Mkopaji atadhaminiwa na wanachama hai wawili au zaidi kutegemea aina na kiwango cha mkopo pamoja na uhalisia wa mazingira ya mkopaji. Kamati ya Mikopo ina haki ya kumwagiza mkopaji kuongeza wadhamini.

(ii) Wadhamini watawajibika kuhakikisha mkopo unalipwa au kulipa mkopo wa mkopaji waliyemdhamini ikiwa mkopo huo hautalipika kwa namna yoyote ile.

(iii) Chama kitakuwa na haki ya kuchukua akiba na hisa za wadhamini kulipia mkopo ambao wameudhamini na haukulipwa na mkopaji.

(iv) Mdhamini mmoja haruhusiwi kudhamini mikopo zaidi ya miwili (2).

## 1.12 ENEO DHAMANA ILIPO

LESA SACCOS Ltd itakubali dhamana za mali isiyohamishika iliyoko ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam tu.

## 1.13 UKOMO WA DHAMANA

Dhamana na udhamini kwa mikopo iliyotolewa na LESA SACCOS LTD itakoma pale ambapo; -

(a) Bakaa ya mkopo ikiwa sawa na bakaa ya akiba za mkopaji.

(b) Wadhamini / mdhamini anapojiondoa au kupoteza sifa za uanachama.

(c) Mkopaji anapokiuka taratibu na masharti ya mkataba wa mkopo.

(d) Mwanachama akikiuka kanuni za maadili kwa mujibu wa kifungu cha 34 na jedwali la pili la Sheria ya Vyama vya Ushirika, 2013 na hivyo kupoteza sifa za uanachama. Katika hali hii, Mwanachama atatakiwa kwa mujibu wa mkataba wa mkopo kurejesha baki ya mkopo wake wote

(e) Kama mkopaji atapata ulemavu wa kudumu, akifariki, kinga ya bima italipia mkopo na riba yote inayodaiwa na chama.

## 1.14 KUJITOA UANACHAMA NA MAEJESHO YA MKOPO

a) Mwanachama mwenye mkopo hataruhusiwa kusitisha uanachama au makato kutoka kwenye mshahara kabla ya kurejesha kiwango chote cha mkopo anachodaiwa. Uongozi wa chama utaridhia kusitisha makato ya kuchangia akiba au marejesho ya mkopo baada ya kujiridhisha kuwa mwanachama anayejitoa uanachama hadaiwi kabisa.

b) Mwanachama anayejitoa uanachama atarejeshewa akiba, mawekezo yake na stahiki nyinginezo kama vile riba na gawiwo endapo limepitishwa na Mkutano Mkuu na kuidhinishwa na Mrajis, hili litafanyika endapo Wanachama wote aliowadhamini hawadaiwi tena au mkopo wao unawiana na akiba/amana zao.

## 1.15 UFUATILIAJI WA MWENENDO WA MIKOPO

a) Meneja wa SACCOS/Mhasibu na watendaji wengine wanao wajibu wa kutunza kumbukumbu zote za wakopaji na kuhakikisha kuwa marejesho ya mikopo yanafanyika kwa kuzingatia mkataba.

b) Kamati ya mikopo itakuwa na jukumu la kupitia taarifa za wakopaji wote katika Vikao vyao vya mara kwa mara.

c) Hati za dhamana na mikataba ya mikopo itatunzwa na Meneja/Mhasibu wa LESA SACCOS Ltd mahali palipo salama.

d) Ikiwa Mwanachama atashindwa kurejesha mkopo kutoka vyanzo vya mshahara kwa kubadilisha mwajiri au kufukuzwa, basi chama kitachukua hatua za kisheria kutumia mali alizonazo Mwanachama ili ziuzwe/kutaifishwa ili kulipia mkopo.

## 1.16 MAOMBI YA MKOPO

(1) Mwanachama ataomba mkopo kwa kujaza fomu inayopatikana kwenye Chama ama kupakua kwenye mtandao/tovuti ya Chama.

(2) Fomu lazima ijazwe kikamilifu na kuwekwa viambatanishi vyote ikiwemo wadhamini kujaza na kusaini sehemu zao kwenye fomu ya mkopo.

(3) Kamati ya Mikopo itahakiki na kuidhinisha mikopo baada ya kuridhia misingi iliyopo inayothibitishausalama wa fedha ya chama itakayotolewa kama mkopo.

(4) Kamati ya mikopo itachanganua na kuweka mikopo yote katika hali ya usalama kwa mujibu wa taratibu zilizopo kabla ya kuidhinisha na kukabidhi maombi yaliyoidhinishwa kwa meneja na Mhasibu ikiwa ni kwa ajili ya kutayarisha malipo kulingana na maamuzi yaliyofanywa na wajumbe wa kamati ya mikopo ua bodi.

(5) Idhini ya mwisho ya mkopo (kutolewa au kutotolewa kwa mkopo) itatolewa na kamati ya mikopo au Bodi nzima kulingana na kiwango cha mkopo

(6) Mwanachama anaweza kukata rufaa ya mkopo wake uliokataliwa kwa Mwenyekiti wa bodi. Mwenyekiti kwa kushauriana na wajumbe wa bodi watatoa uamuzi wa mwisho.

(7) Utaratibu utakaotumika katika utoaji wa mikopo ni aliyeomba kwanza kupewa kwanza (FIRST COME FIRST SERVED BASIS).

## 1.17 KUIDHINISHA NA KUKUBALIWA KWA MAOMBI YA MKOPO

(1) Mikopo yote itatolewa kwa wanachama waliotimiza masharti ya mikopo tu.

(2) Kiwango cha mikopo siyo zaidi ya mara tatu ya baki ya jumla ya akiba na hisa za hiari za mwanachama.

(3) Maombi ya mkopo kwa hatua za mwanzo yatapokelewa na Afisa mikopo au Mhasibu na baadaye kupelekwa kwenye kamati ya mikopo au Bodi kwa hatua ya kujadiliwa na kuidhinisha.

(4) Maombi yote ya mikopo yatafanyika kwa kutumia fomu maalum na ni lazima kwa kila hali fomu ielezee:-

i. Kiasi cha mkopo kilichoombwa.
ii. Madhumuni ya mkopo.
iii. Kiwango cha madeni anayodaiwa mkopaji.
iv. Dhamana ya mkopo.

(5) Mikopo itakuwa inapitishwa na Kamati ya mikopo au Bodi kwa kufuata utaratibu wa aliyekuja kwanza kuhudumiwa kwanza (FIRST COME FIRST SERVED BASIS).

## 1.18 MAMLAKA YA KUIDHINISHA MIKOPO

(a) SACCOS haitatoa mkopo bila idhini ya kamati ya mkopo
(b) Kamati ya mikopo haitaidhinisha mkopo kama sehemu ya mkopo haijazaminiwa au mkopo haujazaminiwa kikamilifu
(c) Kamati ya mkopo itaridhia ombi la mkopaji kupewa mkopo baada ya kujiridhisha na uwezo wa mwanachama kufanya marejesho
(d) Kamati ya mikopo ina haki ya kukataa/kukubali au kurudisha ombi la mkopo kwa mwanachama ikiwa mwanachama atakuwa hakutimiza vigezo vya kupewa mkopo kama ilivyoelekezwa katika sehemu ya 2.1 ya sera hii.
(e) Ikiwa ombi la mkopo halijakubaliwa SACCOS itamfahamisha mwanachama sababu za kukatatiliwa kwa ombi lake ndani ya kipindi cha siku saba.
(f) Fedha za mikopo zitatolewa kutegemeana na hali ya ukwasi chamani lakini kwa namna yeyote ile mikopo midogo itapewa kipaumbele na ikiwa hali ya ukwasi wa chama iko chini.
(g) Meneja wa chama ataruhusiwa kuidhinisha mikopo yote ya dharura na chap chap kwa wanchama wenye sifa za kukopa mara baada ya afisa mikopo kujiridhisha uwezo wa mkopaji katika kurejesha mkopo husika wa dharura
(h) Kamati ya mikopo/kamati ya kitaalam itatumia kumbukumbu zifuatazo ili kufikia uamuzi wake;

i) Mali anazotumia mwanachama kudhamini mkopo
ii) Daftari linaloonyesha orodha ya wanachama
iii) Uzoefu katika shughuli anayoombea mkopo
iv) Aina ya mradi unaoombewa mkopo
v) Mahali mradi ulipo
vi) Pamoja na vigezo vingine vitakavyowekwa na chama.
vii) Kanuni ya 30 ya kanuni za huduma ndogo za fedha – SACCOS za mwaka 2019

## 1.19 MIKOPO KWA VIONGOZI NA WATENDAJI

i. Viongozi wanasifa ya kupatiwa mikopo kwa taratibu sawa na Wanachama wengine bila upendeleo wowote.
ii. Jumla ya mikopo yote kwa Viongozi na Watendaji haitakiwi kuzidi 5% ya rasilimali za Chama.

### *Viwango vya mikopo na uidhinishaji*

### Uidhinishaji wa kamati ya mikopo

Uidhinishaji wa mikopo utakua chini ya kamati ya mikopo au kamati ya kitaalam na kamati ya mikopo au kamati ya kitaalam haitaidhinisha mkopo unaozidi kiasi cha shilingi 100,000,000

### Uidhinishaji wa meneja

LESA SACCOS LTD Meneja atakuwa na mamlaka ya kuidhinisha mikopo yote ya dharura isiyozidi kiasi cha.10,000,000 baada ya afisa mikopo kujiridhisha kama mkopaji anaweza kufanya marejesho kwa mkopo huo, mikopo mingine itafata taratibu zilizoainishwa katika sera hii.

### *Mikopo kwa watendaji wa chama*

i. SACCOS itatoa mikopo kwa watendaji kulingana na sera ya mikopo ya rasilimali watu tu.
ii. SACCOS haitatoa mkopo kwa mtendaji au mtu mwenye mahusiano ya karibu na chama kwa namna yeyote ile kabla ya kupata idhini kutoka kwa kamati ya mikopo.

iii. Mikopo ya watendaji wakuu wa SACCOS lazima ijadiliwe na bodi ya chama na kamati ya mikopo kabla haijapata idhini.

## 1.20 KUREJESHA MIKOPO

(a) Kwa zaidi ya 97% ya marejesho ya mikopo kwa Wanachama yatafanyika kwa mfumo wa makato ya moja kwa moja kwenye mshahara wa mwanachama kupitia muajiri.Aidha, mwanachama anawezakufanya marejesho ya mkopo pamoja na riba kwa kulipa fedha taslimu kwenye Chama ama kupitia akaunti ya chama na kuwasilisha "payslip" ya benki ofisi ya LESA SACCOS Ltd wakati wa saa za kazi.

(b) *Taarifa juu ya maendeleo* ya mikopo zitaandaliwa na Afisa Mikopo kila mwezi kwa ajili ya matumizi ya Menejimenti na kila robo mwaka kuandaliwa na Kamati ya Mikopo kwa kusaidiana na Afisa Mikopo na Meneja na kuwasilishwa kwenye vikao vya Bodi kila robo mwaka.

## 1.21 MUDA NA UTARATIBU WA MAREJESHO

(1) Ukomo wa marejesho usiozidi muda wa miezi 12 hadi miezi 60 kulingana na aina na kiasi cha mkopo. Aidha, kutokana na hali ya ushindani katika soko la fedha, Bodi inapewa nguvu na Sera hii kubadilisha muda wa juu wa urejeshwaji mkopo ili kukidhi mahitaji ya soko na Wanachama kwa wakati husika.

(2) Utaratibu wa marejesho kwa mikopo yote (msingi na riba) *utakuwa ni malipo ya* Kila baada ya wiki mbili.

## 1.22 MENEJIMENTI YA MAJANGA YA MIKOPO

### *Gharama za kinga ya majanga ya Mkopo*

LESA SACCOS LTD itatoza kiasi cha 2% katika kila mkopo unaochukuliwa isipokuwa mkopo wa dharura na kiasi hicho kitahifadhiwa katika akaunti maalum kwa lengo la kulinda mikopo ambayo haitarejeshwa kutokana na sababu zifuatazo;

i. Ikiwa mwanachama amefariki akiwa hajamaliza mkopo na chama kimethibitisha kuwa kwa namna yeyote mkopo ulioachwa hauwezi kulipika.

ii. Ikiwa mwanachama amepata ulemavu wa kudumu na imepelekea kushindwa kutekeleza majukumu yake ya kumwingizia kipato na hatimaye kushindwa kulipia mikopo anayodaiwa

iii. Ikiwa mwanachama ana ugonjwa wa akili na hawezi kutoa ushirikiano katika kufanya marejesho kwa mujibu wa mkataba wake na daktari wa serikali amethibitisha juu ya ugonjwa wa akili wa mwanachama husika.

2. *Taratibu za kuhudumia mfuko wa bima*

a. Fedha za mfuko wa bima ya mkopo zitawasilishwa benki katika akaunti maalum mara baada ya mwanchama kupatiwa mkopo

b. Fedha za mfuko zitatumika kwa malengo yaliyokusudiwa kwa kuzingatia mahitaji yatayojitokeza.

c. Ikiwa mfuko haujaimarika vya kutosha kuweza kumudu mahitaji yanayojitokeza kiasi kinachodaiwa kinaweza kusubiri mfuko uimarike ndipo kilipwe

## 1.23 NJIA YA KUKOKOTOA RIBA

Riba kwa aina ya mikopo yote itakokotolewa kwa njia ya baki ya mkopo (reducing balance).

## 1.24 UFUATILIAJI WA MAREJESHO YA MKOPO

(a) Kila mwanachama ana wajibu kuhakikisha kuwa marejesho ya mikopo aliyochukua yanafanyika kama ilivyokubaliwa.

(b) Afisa Mikopo atahusika mara kwa mara kutengeneza taarifa ya hali halisi ya mikopo kila mwezi.

(c) Taarifa zitaonyesha hali halisi ya maendeleo ya mikopo na zitawasilishwa mbele ya Bodi kila baada ya miezi mitatu.

## 1.25 UKOKOTOAJI NA UAINISHAJI MIKOPO ILIYOCHELEWESHWA

Chama kinapaswa kuandaa taarifa za ukokotoaji wa mikopo iliyocheleweshwa kwa kuanzia tarehe ya mwisho ambayo rejesho la mkopo husika lilifanyika mpaka pale malipo yote yatakapokuwa yamekamilika. Mikopo iliyocheleweshwa itakokotolewa kila mwezi na kutolewa taarifa siku ya mwisho wa mwezi ambapo mikopo hiyo itaainishishwa katika makundi yafuatayo:-

**Jedwali Na.3 Makundi na Hali ya Ucheleweshaji.**

| Na. | Makundi ya Uchelewaji | Hali ya Uchelewaji |
|---|---|---|
| 1. | Mikopo iliyopo kwenye angalizo | Siku 31-90 |
| 2. | Mikopo iliyo chini ya Kiwango | Siku 91-180 |
| 3. | Mikopo yenye mashaka | Siku 181-365 |
| 4. | Mikopo mibaya/Hasara | Zaidi ya siku 365 |

### Taarifa muhimu zinazopaswa kuainishwa kwa mikopo iliyocheleweshwa

Taarifa ya ucheleweshwaji wa mikopo itajumuisha mambo yafuatayo;

i. Jina la mwanachama, anuani na mawasiliano yake binafsi
ii. Tarehe mkopo ulipotolewa
iii. Mkopo halisi uliotolewa na bakaa la deni linalodaiwa ambalo halijarejeshwa chamani
iv. Majina ya wadhamini na dhamana ya mkopo iliyowekwa na

## 1.26 USITISHAJI WA MAPATO TARAJIWA NA MAREKEBISHO YA MKOPO

### Kusitisha mapato tarajiwa kutokana na mikopo iliyocheleweshwa

Chama kitasitisha riba zote tarajiwa ambazo zitakuwa zimekadiriwa kupatikana kwenye mwaka husika kutokana na mikopo iliyocheleweshwa iwapo mkopo uliotolewa hautalipwa kwa siku tisini. Aidha, chama kitaondoa mapato tarajiwa yanayotokana na mikopo kutoka katika akaunti ya mapato tarajiwa.

## 1.27 MADENI, MATENGO NA USIMAMISHAJI WA MIKOPO KWA MUDA

### Madeni Mabaya

(a) Madeni mabaya ni yale yatakayokuwa yameshindwa kurejeshwa katika kipindi kinachozidi siku 30 kama ilivyofafanuliwa katika kanuni ya 40 (1)(2) ya kanuni za huduma ndogo za fedha (SACCOS) za mwaka 2019

(b) Madeni mabaya yatafutwa katika mahesabu ya chama yatakapokuwa yamefikia zaidi ya miezi kumi na mbili (12) kwa kuzingatia Kanuni ya 43 ya kanuni za SACCOS za mwaka 2019.

(c) Chama kitaendelea kufuatilia madeni hayo na yakilipwa yataingizwa kama mapato mengineyo kwa kuzingatia taratibu za kihasibu.

### 2. Matengo ya madeni mabaya

Chama kitafanya matengo ya mikopo mibaya kwa kuzingatia kanuni Na. 40(3) ya kanuni za huduma ndogo za fedha za mwaka 2019.
LESA SACCOS LTD itatenga kiasi toshelevu cha fedha kutoka katika faida yake ya mwaka kwa ajili ya kufidia mikopo mibaya iliyocheleweshwa na wanachama kwa kuzingatia kanuni Na. 40(3) ya kanuni za huduma ndogo za Fedha (SACCOS) za mwaka 2019 ili kufidia kiasi cha mikopo hiyo mibaya kama inavyoainishwa katika jedwali Na.2

**Jedwali Na.2 Matengo ya Mikopo Mibaya.**

| Na. | Makundi ya Uchelewaji | Hali ya Uchelewaji | Kiasi cha matengo(% ya bakaa kwa mkopo uliochelewa) |
|---|---|---|---|
| 1. | Mikopo iliyopo kwenye angalizo | Siku 31-90 | 10% |
| 2. | Mikopo iliyo chini ya Kiwango | Siku 91-180 | 30 |
| 3. | Mikopo yenye mashaka | Siku 181-365 | 50 |
| 4. | Mikopo mibaya/Hasara | Zaidi ya siku 365 | 100 |

**Kiasi cha tengo litakalotengwa kwa ajili ya kufidia mikopo mibaya iliyocheleweshwa kitawekwa kwenye akaunti maalum ya mikopo mibaya.**

3. Kusimamisha mikopo kwa muda

(a) Chama kinaweza kusimamisha utoaji wa mikopo kulingana na mwenendo wa ulipaji wa mikopo hiyo.

(b) Ikiwa na Mikopo mingi ambayo ipo mikononi mwa wanachama na haijakusanywa na hivyo kuhatarisha hali ya ukwasi katika chama "liquidity crisis".

(c) Endapo Mrajis wa Vyama vya Ushirika atafanya ukaguzi na kubaini na kujiridhisha kuwa hali halisi ya kifedha ni mbaya.

## 1.28 TAARIFA ZA MIKOPO

Taarifa za mikopo ni moja ya nyenzo ya menejimenti ya mikopo na ni hatua ya kwanza kabisa kutambua aina, idadi, kiwango na thamani ya mikopo iliyocheleweshwa kulingana na umri. Hivyo, taarifa ya mikopo sharti iandaliwe kila mwezi, robo mwaka, nusu mwaka na kila mwaka na Afisa Mikopo, Meneja, Kamati ya Mikopo na Bodi ya Chama.

## 1.29 TARATIBU ZA KUFUATILIA MIKOPO ILIYOCHELEWA

Taratibu zifuatazo zitafuatwa kufuatilia madeni:-

i) Mkopo uliochelewa siku 1-30: Mwanachama atakumbushwa kwa simu na wadhamini wake juu ya kuheshimu mkataba wa mkopo kwa kufanya marejesho yake yanayochelewa. Kila wiki ndani ya siku 30 kukumbushwa kwa simu kutafanywa na Afisa Mikopo.

ii) Mkopo ukiendelea kuchelewa zaidi ya siku 30: Barua za kumkumbusha zitaanza kutolewa kama ifuatavyo:

1. Barua ya kwanza (demand note) kwa mkopaji na wadhamini wake ikiwa ni taarifa na kupewa muda wa siku 14 awe amefanya marejesho yake.

2. Kama ndani ya muda siku 14 hakuna kilichofanyika barua ya pili (demand note) kwa mkopaji na wadhamini na kupewa muda wa siku 14 tena kuwa wamefanya marejesho.
3. Kama ndani ya siku 14 za pili hakuna mwitikio wowote, barua ya tatu kwa mkopaji na wadhamini ikionesha kupewa siku 14 nyingine na endapo atashindwa kufanya marejesho yake hatua za kisheria zitafuata ikiwa ni pamoja na kuanza mchakato wa kutumia na kuuza dhamana kulipia mkopo.
4. Kama ndani ya siku 14 kwa mara ya tatu hakuna kilichofanyika, barua ya kisheria itaandikwa kumtaarifu mkopaji na wadhamini kuanza kwa zoezi la kutumia na kuuza dhamana zao (wote Mkopaji na Wadhamini) kulipia mkopo. Chama kitaanza kuuza dhamana za mdhamini na endapo hazitoshelezi kulipa deni la mkopo wote, Chama kitaendelea na dhamana za wadhamini.
5. Hatua za kuchukua akiba za mkopaji na wadhamini kulipia mkopo zitaanza, kama bado mkopo haujalipwa kwa ukamilifu, zoezo la kuuza mali nyingine zilizowekwa kama dhamana zitauzwa.

## 1.30 UKUSANYAJI WA MADENI

Mikopo yote itakayotolewa na chama kwa wanachama wake itapaswa kulipwa chamani kwa utaratibu uliopangwa na ikiwa utataratibu uliowekwa hautafatwa na wakopaji chama kitakuwa na jukumu la kufatilia na kuhakikisha madeni yote yanakusanywa.

### 1.Mambo ya kuzingatia kabla ya kuanza ukusanyaji wa madeni

Chama kitaendelea kuhakikisha madeni yote yanakusanywa kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa kati ya mkopaji na mkopeshaji na mambo yafuatao yakibainika ufatiliaji wa karibu utahitajika, aidha miongoni mwa mambo hayo ni pamoja na;

i. Malipo ya marejesho ya mwanachama yatakuwa pungufu ya malipo yaliyotakiwa kulipwa kwa mujibu wa masharti ya mkataba uliosainiwa na mwanachama kipindi anachukua mkopo.
ii. Endapo malipo ya marejesho ya mwanachama hayatafanyika ndani ya kipindi cha siku thelathini (30) tangu marejesho hayo kutakiwa kufanyika bila kujali kuwa mkopo uliocheleweshwa ni riba au riba na mkopo msingi.
iii. Iwapo Jedwali la marejesho ya Mkopo lililopo kwenye fomu ya mikopo halitazingatiwa katika marejesho ya mkopo ya mwanachama.

## 2. Mkataba wa mkusanya madeni

Chama kinaweza kuingia mkataba na mkusanya madeni endapo itaonekana mkopaji amecheleweshа marejesho na jitihada za chama kufanya ufatiliaji zimeshindwa kuzaa matunda na hatimae kuona umuhimu wa kuweka mkusanya madeni.

Aidha chama kinapaswa kuzingatia mambo yafuatayo kabla ya kuingia mkataba na mkusanya madeni;

i. Kuhakikisha mkusanya madeni ana kibali maalum cha kufanya kazi hiyo kutoka mamlaka halali za serikali
ii. Kujiridhisha mahali na sehemu mtoa huduma anafanyia kazi zake
iii. Kuangalia historia ya mtoa huduma
iv. Kuhakikisha mtoa huduma ana linda haki za mwachama wakati wa kukusanya madeni
v. Kuhakikisha mkusanya madeni anakusanya deni kwa kuzingatia mkataba na makubaliano yaliyopo kwenye fomu ya mkopo na mkataba wa mkopo
vi. Kuhakikisha mkusanya madeni anatambua vema mali za mkopaji zilizotumika kudhamini mkopo
vii. Kufanya tathmini na kujirdhisha kama Kuhakikisha mkusanya madeni ana uwezo na vifaa vitakavyomsaidia kufanya kazi hiyo pasipo kungiza chama gharama

viii. Mkataba uainishe haki na wajibu za pande zote na upite kwa mwanasheria kwa ajili ya kulinda haki za pande zote

ix. Mkataba wa mkusanya madeni na chama unapitishwa kwa Mrajis ili aone kama mkataba husika haujaegemea upande mmoja

## 1.31 HAKI JUU YA DHAMANA

LESA SACCOS Ltd ina haki juu ya dhamana yoyote iliyowekwa na mkopaji na wadhamini wake. Hivyo, Chama kitaamua ni dhamana ipi (kati ya zile za mkopaji na wadhamini) inaweza kuwa ya kwanza kutumika kufidia mkopo kulingana na wepesi, changamoto mbalimbali na gharama zinazohusiana na zoezi la kutumia dhamana kulipia mkopo.

## 1.32 UFUTAJI MIKOPO NA UUZAJI WA DHAMANA

### 1. Hatua za ufutaji wa mikopo

LESA SACCOS LTD itafuta mikopo yake kutoka katika mizania yake endapo:

(a) Mkopo utacheleshwa kurejeshwa kwa zaidi ya siku 365;

(b) Chama kitapoteza haki zake za kimkataba zinazohusiana na mkopo husika;

(c) Chama kimekosa haki kisheria katika dai la mkopo husika

(d) Mkopo utakapoonekana hauwezi kukusanywa;

(e) Hakuna uwezekano wa chama kukusanya mkopo kutokana na hukumu ya mahakama.

(f) Dhamana zote zilizodhamini mkopo, zimetathiminiwa na kuuzwa, na mapato yanayotokana na mauzo yameshindwa kufuta mkopo unachodaiwa

(g) Chama hakina uwezo wa kukusanya mkopo au hakuna dhamana au jitihada za kukusanya deni zimeshindikana.

(h) Ikiwa chama kina tengo la mikopo mibaya linalotosha kufuta mkopo

**Iwapo mkopo wa mwanachama utafutwa kwenye vitabu vya chama na kama mwanachama huyo atakuwa**

**hajatangazwa kufilisika, mkopo huo utapaswa kufuatiliwa na kukusanywa kama mikopo mingine.**

## 2. Taratibu za chama kuuza dhamana za mwanachama

Ili kufidia mikopo mibaya chama kinaweza kuuza dhamana za mwanachama. Aidha Kabla chama hakijauza dhamana za mwanachama kitapaswa kuzingatia mambo yafuatayo;

i. Akiba, amana na hisa za hiyari za mwanachama zimechukuliwa katika akaunti ya mwanchama lakini hazijatosheleza kulipa deni husika la mwanchama
ii. Wadhamini wamepatiwa taarifa na kushindwa kutoa ushirikiano wa kutosha kuhakikisha deni la mkopaji limelipwa.
iii. Ikiwa mwanachama ana dhamana zaidi ya moja dhamana itakayouzwa ni ile tu inayoweza kukidhi deni husika na dhamana zilizobaki zinaweza kurudishwa baada ya kujiridhisha deni husika limelipwa kikamilifu.
iv. Chama kitalazimika kurudisha kiasi cha fedha kilichobakia mara baada ya dhamana kuuzwa na kufuta mopo
v. Chama kinaweza kuuza dhamana za mdhamini baada ya akiba, hisa na dhamana za mkopaji mwenyewe kushindwa kulipia mkopo

Kwa mujibu wa Kanuni ya 79(5) ya SACCOs ya Mwaka 2014, taarifa za mikopo iliyofutwa ni siri ya ndani ya Chama, hivyo, taratibu za ufuataji mkopo ni kama ifuatavyo:

i) Taarifa ya Meneja kwenda Bodi itaandikwa ikianisha kila mkopo kiasi kilichoidhinishwa, tarehe, marejesho yalifanyika, alibaki ya mkopo siku za kuchelewa, hatua zilizochukuliwa, sababu za kupendekeza kufutwa.
ii) Bodi watajadili na kufanya maamuzi.
iii) Baada ya Bodi kufanya maamuzi ya kufuta mikopo husika na muhtasari kuandikwa Mhasibu atafanya zoezi la kufuta mikopo iliyoidhinishwa na Bodi kufutwa kwa kupunguza thamani ya mikopo na kupunguza pia tengo la madeni mabaya kama tengo hilo lina fedha za kutosha kubeba kiasi cha mikopo inayofutwa.

iv) Kama tengo la madeni mabaya halina fedha za kutosha kufuta mikopo basi kiasi cha mkopo unaofutwa kilichoshindikana kufutwa kupitia tengo la madeni mabaya kitaingizwa kwenye matumizi ya kawaida ya Chama kupitia Kasma ya tengo la madeni mabaya.

v) Ni vizuri Bodi kuwasiliana na Mrajis Msaidizi wa Mkoa kwa kila hatua kabla na baada ya kufuta mikopo vitabuni. Hii ni kwasababu za kiuwajibikaji kwa Mamlaka ya usimamizi wa Sheria lakini pia Chama kinaweza kupata ushauri wa busara na njia mbadala kutoka Ofisi ya Mrajis kabla ya kufuta mikopo vitabuni.

## 1.33 UFUATILIAJI MKOPO BAADA YA KUFUTWA VITABUNI

Zoezi la kufuta mikopo si sababu ya kumsamehe mkopaji wala Bodi kuacha ufuatiliaji bali hii ni taratibu za kiuhasibu tu kusafisha vitabu na hivyo mwanachama lazima aendelee kutafutwa na kudaiwa mkopo husika kwa mbinu na namna yeyote ile. Endapo atarejesha, fedha hizo zitaingizwa kwenye mapato ya Chama kama Mapato yatokanayo na Mikopo iliyofutwa.

## 1.34 NAFASI YA MAHAKAMA KUPITIA TARATIBU ZA TUME

Chama kinaweza kufungua kesi Mahakamani kupitia Wanasheria wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania kama kuna tatizo ama mgogoro wowote kwenye dhamana ama Mwanachama mkopaji amekimbia bila kujulikana alipo. Chama kitafungua kesi ili kupata hati ya mahakama ya kukamata mali zozote za mkopaji na kuuzwa ili kufidia mkopo.

## 1.35 MAREKEBISHO YA MKOPO

LESA SACCOS LTD haitafanya marekebisho ya mkopo zaidi ya mara moja kwa wanachama wake watakaopewa mikopo na kushindwa kurejesha kwa wakati.

i. Mkopo wowote ambao umefanyiwa marekebisho au mabadiliko katika masharti yake ya awali, hautapaswa kuainishwa kama "upo katika daraja zuri" isipokuwa marejesho ya mkopo huo yamefanyika kikamilifu angalau mara nne mfululizo tangu mkopo ulipofanyiwa marekebisho.

ii. iwapo mkopo utafanyiwa marejesho kikamilifu mara nne mfululizo, mkopo huo utaainishwa kama mkopo usiocheleweshwa.

iii. LESA SACCOS LTD itatoa taarifa ya mikopo yote iliyofanyiwa marekebisho kama taarifa inayojitegemea katika mizania ya hesabu ya chama.

Kanuni ya 42(1) ya kanuni za huduma ndogo za fedha inaruhusu Chama kufanya marekebisho ya Mkopo( Loan Restructuring) pale tu ambapo kuna uhakika kuwa kwa kufanya hivyo kutamsaidia mwanachama kuendelea kurejesha vizuri mkopo wake.

Marekebisho ya mkopo (restructuring) ni hali ya kuongeza muda wa mkopo ili kupunguza kiwango cha marejesho kwa mwezi, kumwezesha mwanachama kufanya marejesho kulingana na kiwango anachoweza kwa wakati husika.

Kabla ya kurekebisha mkopo sharti mwanachama alipe riba yote ambayo imelimbikizwa na msingi wa mkopo ndiyo unaweza kufanyiwa marekebisho.

Mkopo uliofanyiwa marekebisho utaendelea kukaa katika kundi la Chini ya kiwango hadi pale mwanachama atakapokuwa amefanya marejesho mara sita (6) mfululizo ndiyo utahamishwa kwenda kundi la kiwango.

## 1.36 *Uidhinishwaji wa Sera*

Sera hii imetayarishwa na kupitishwa na Bodi ya LESA SACCOS LTD kwa niaba ya wanachama kwa kibali cha Mrajis katika kikao chake kilichofanyika tarehe 17 Julai 2020 na itaanza kutumika

baada ya kuidhinishwa na kusajiliwa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika.

............................
**Mwenyekiti**

............................
**Meneja**

LEA SAVINGS & CREDIT COOPERATIVE SOCIETY LTD.
23 NOV 2020
KINONDONI
DAR ES SALAAM

............................................
**Mrajis wa Vyama vya Ushirika**

Tarehe............................

TANZANIA
Approved this 20TH
day of JANUARY 2021
............
Asst. Registrar of Cooperative Societies